





Je, Wanajua

Uelewa wa wapiga kura



Ufahamu wa Tume ya Uchaguzi (NEC)

Asilimia 62 ya wananchi waliweza kulitaja kwa usahihi jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kama chombo kitakachosimamia uchaguzi mkuu Tanzania bara.



Kielelezo cha 1: Je, ni chombo gani kitakachosimamia uchaguzi mkuu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Chanzo cha takwimu: Sauti za Wananchi – Awamu ya 34 (Juni 2015)

Asilimia 51 wana imani na uwezo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

Kwa kiwango gani unaamini utendaji wa NEC katika kuhakikisha uchaguzi mkuu ujao 2015 utakuwa huru na wa haki?



Kielelezo cha 2: Ni kwa kiwango gani unaiamini kazi ya NEC?

Chanzo cha takwimu: Sauti za Wananchi – Awamu ya 34 (Juni 2015) Majibu ya "Sijui" na wasiojibu hayajumuishwa hapa.

Asilimia 53 wameusikia mfumo mpya wa kuandikisha wapiga kura (BVR). Miongoni mwao, asilimia 63 wanaona ni mfumo huu ni bora kuliko mfumo wa zamani.

Vile vile, wananchi waligawanyika kwenye kutathmini utendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa uchaguzi wa mwaka 2010.

Elimu ya wapiga kura mwaka 2010

49%

34%

15%

Mienendo ya wafanyakazi na usaidizi kwa wananchi mwaka 2010

52%

34%

13%

Kuendesha upigaji kura siku ya uchaguzi mwaka 2010

54%

33%

12%

Usahihi wa matokeo mwaka 2010

54%

33%

12%

Kutangaza matokeo kwa wakati mwaka 2010

54%

31%

13%

Kubadika majina ya wapigakura mwaka 2010

56%

31%

12%

Uandikishaji wa wapigakura mwaka 2010

58%

31%

9%

0% 10% 20% 30% 50% 60% 70% 80% 90% 100%

Kielelezo cha 3: Ni kwa kiasi gani ni unaridhika na utendaji kazi wa NEC kwenye maeneo yafuatayo wakati wa uchaguzi uliopita wa mwaka 2010

Chanzo cha takwimu: Sauti za Wananchi – Awamu ya 34 (Juni 2015) Majibu ya "Sijui" na wasiojibu hayajumuishwa hapa.

Muhtasari huu umeandaliba na Twaweza East Africa.

Umetolewa Septemba 2015

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.

+255 22 266 4301 uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Huru na Haki?

Hata hiyo wananchi hawaamini kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu utafanyika kwa uhuru na haki.

Asilimia 65 ya wananchi wanaamini kuwa mgombea mwenye sera nzuri atashinda, ikilinganishwa na asilimia 35 wanaoamini kuwa mgombea mwenye fedha ndiye atakayeshinda.




Asilimia 76 ya wananchi wanafikiri vyombo vya habari vitaripoti kwa usahihi na kwa haki juu ya uchaguzi mkuu, wakati asilimia 24 wanadhani vitaegemea upande wa wagombea fulani kutokana upendeleo au kupewa fedha.

Asilimia 18% wanafikiri kuwa viongozi walio madarakani watavunja sheria ili washinde uchaguzi.

Hata hivyo, wakiwa na wasiwasi, asilimia 54 ya wananchi wanaona kuwa uwezekano mkubwa upo wa kutokea vurugu wakati wa uchaguzi.

Sheria za kampeni ni zipi?


Wananchi 3 kati ya 4 wanafahamu kuwa kugawa fedha au chakula na vinywaji katika mikutano ya kampeni ni kinyume cha sheria. Hata hivyo, wananchi wanaona kuwa siyo sahihi kwa vyama vya siasa na wagombea kutunza kumbukumbu za michango na matumizi yake.



Chanzo cha takwimu: Sauti za Wananchi – Awamu ya 34 (Juni 2015) Majibu ya "Sijui" na wasiojibu hayajumuishwa hapa

Sifa za wagombea Urais?

Wakati kuchagua Rais, wananchi wataangalia zaidi sera, na sio dini za wagombea wala utajiri wao.



Kielelezo cha 5: Ni sifa gani MUHIMU utakayozingatia zaidi wakati wa kumchagua Rais?

Wananchi wamegawanyika kuhusu ubora wa viongozi wa serikali tangu mwaka 1961; asilimia 44 wanasema ubora umeshuka, wakati asilimia 43 wanafikiri ubora umeongezeka.

Mbinu ya utafiti

Takwimu zimetokana na awamu ya 34 ya Sauti za Wananchi, utafiti wa kwanza barani Afrika wenyewe uwakilishi wa kitaifa unaofanyika mara kwa mara kwa njia ya simu za mkononi. Takwimu zilikusanywa kwa wahojiba 1,335 Tanzania Bara (Zanzibar haimo) kati ya tarehe 12 na 26 Juni 2015.